# HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA

## MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA KILICHOKETI TAREHE 27/10/2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Dormohamed I. Rahmat | - | Mstahiki Meya (Mwenyekiti) |
| 2. | Mhe. Agness P. Mangasila | - | Naibu Meya |
| 3. | Mhe. Dr. Tulia Ackson | - | Mbunge Jimbo la Mbeya Mjini |
| 4. | Mhe. David P. Mwashilindi | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Juma S. Simbeyanje | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Daudi N. Ngogo | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Zabibu I. Kimata | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Mwajuma A. Tindwa | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Fatuma C. Bora | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Sambwee Shitambala | - | Mjumbe |

**WATAALAMU WALIOHUDHURIA: -**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Triphonia Kisiga | - | Kaimu Mkurugenzi wa Jiji – Katibu |
| 2. | Zena Kapama | - | Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 3. | Sisty Chibby | - | kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi |
| 4. | Mpakani Kalinga | - | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 5. | Gregory T. Emmanuel | - | Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi |
| 6. | Dkt.Jonas Lulandala | - | Mkuu wa Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii |
| 7. | Gilbert M. Nkoronko | - | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA |
| 8. | Bosco Komba | - | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |
| 9. | Dkt. Lawrence Kibona | - | Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi |
| 10. | Amiri A. Hamza | - | Afisa Usafirishaji |
| 11. | Mashaka Semkiwa | - | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| 12. | Amina Nalicho | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika |
| 13. | Oswald Kasambala | - | Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 14. | Ally M. Liuye | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 15. | Emmanuel Kimbe | - | Mratibu wa TASAF/Katibu wa Timu ya Mbeya City |
| 16. | Hajayand Adon | - | Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango,Takwimu na Ufuatiliaji |

**SEKRETARIETI**

1. Nickson G. Massoko
2. Stella Jackson
3. Joseph Mlundi

**AGENDA**

1. Kufungua Kikao.
2. Kuridhia Agenda.

3. Taarifa ya Mapokezi ya Fedha kiasi cha Tsh. 1,840,000,000.00 za mgao wa ujenzi wa Vyumba vya madarasa kwa ajili ya Kidato cha Kwanza mwaka 2022 kupitia Mradi wa kupunguza athari za Uviko – 19 katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya na mkakati wa utekelezaji wake.
   a) Maombi ya kufanya mabadiliko ya vifungu vya fedha kiasi cha Tsh. 100,000,000/= kutoka Mapato ya Ndani.
   b) Uhamisho/Kuongeza vifungu katika bajeti ili kuweza kutumia Fedha zilizotolewa kwa ajili ya kutekeleza mradi Na.5441- TANZANIA COVID – 19 SOCIAL ECONOMIC RECOVERY AND RESPONSE PLAN kupitia Fedha za mkopo nafuu wa (IMF) INTERNATIONAL MONETARY FUND
4. Kufunga Kikao.

**MCC/FU/01/2021/2022 KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao baada ya akidi kutimia na akawaeleza Wajumbe kwamba ni Kikao Maalum cha kupokea Taarifa ya Mapokezi ya Fedha kiasi cha Tsh. 1,840,000,000.00 za mgao wa ujenzi wa Vyumba vya madarasa kwa ajili ya Kidato cha Kwanza mwaka 2022 kupitia Mradi wa kupunguza athari za Uviko – 19 katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya na mkakati wa utekelezaji wake.

Akifungua Kikao Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe kwa kuhudhuria na akawaomba kufanikisha Kikao.Baada ya kusema hayo alifungua Kikao saa 2:30 Asubuhi.

**MCC/FU/02/2021/2022 KURIDHIA AGENDA**

Mwenyekiti aliwahoji Wajumbe kama wanaridhia agenda zilizowasilishwa ili zijadiliwe katika Kikao hicho.

Wajumbe kwa kauli moja waliridhia agenda zote zijadiliwe.

**MCC/FU/03/2021/2022 TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA KIASI CHA TSH. 1,840,000,000.00 ZA MGAO WA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA KWA AJILI YA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2022 KUPITIA MRADI WA KUPUNGUZA ATHARI ZA UVIKO – 19 KATIKA HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA NA MKAKATI WA UTEKELEZAJI WAKE.**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji ndugu Hajayand Adon aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha kiasi cha Shs. 1,840,000,000.00 za mgao wa ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya Kidato cha Kwanza mwaka 2022 kupitia mradi wa kupunguza athari za Uviko – 19 katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya na mkakati wa utekelezaji wake na kueleza kuwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya imepokea kiasi hicho ambazo zimeingizwa moja kwa moja kwenye akaunti za shule. Mwisho aliwasilisha Orodha ya Shule pamoja na Madarasa kwa kila shule na kiasi cha fedha kilichopelekwa kwa kila shule.

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo, Wajumbe walipokea na kujadili kama ifuatavyo:-

Mhe. Davidi Mwashilindi alitoa pongezi kwa Serikali kwa kuipatia Halmashauri fedha hizo. Aidha alishauri kuwa pindi fedha zinapofika ni vyema kuwe na utaratibu wa Wahe. Madiwani kupewa taarifa.

Mhe. Juma Simbeyanje alihoji kuhusu Serikali Kuu kuipatia fedha za ujenzi kwa shule ya Itagano, Itende na Mabatini.
Ufafanuzi ulitolewa na Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji ndugu Hajayand Adon kuwa ujenzi wa shule ya Itagano, Itende na Mabatini utatumia makusanyo ya Mapato ya Ndani.

Mhe.Mbunge. Dkt. Tulia Acksona alishauri kuwa ni vyema iwasilishwe taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa shule ya Sekondari Itende na shule ya Sekondari Itagano. Aidha alishauri kuwa ni vyema kufanyike utaratibu wa kutafuta eneo linguine la uanzishaji wa shule ya Sekondari Iyela.

Baada ya majadiliano hayo, Wajumbe wa Kamati ya fedha na Utawala walisisitiza kuwa kufanyike utaratibu wa kupeleka fedha mapema na kwa wakati za ujenzi wa shule ya Sekondari ya Itende, shule ya Sekondari ya Itagano na shule ya Sekondari Mabatini kupitia fedha za makusanyo ya Mapato ya Ndani. Aidha katika Kikao kijacho cha Kamati ya Fedha na Utawala cha mwezi Novemba 2021 iwasilishwe taarifa ya hatua iliyofikiwa ya usajili wa shule ya Sekondari ya Itende na shule ya Sekondari ya Itagano. Pia ifanyike ziara ya kutembelea eneo linalotarajiwa kujengwa shule ya Sekondari Iyela.

**AZIMIO**

1. Kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala kilijadili na kuazimia kwamba kufanyike utaratibu wa kupeleka fedha mapema na kwa wakati za ujenzi wa shule ya Sekondari ya Itende, shule ya Sekondari ya Itagano na shule ya Sekondari Mabatini kupitia fedha za makusanyo ya Mapato ya Ndani.
2. Kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala kilijadili na kuazimia kwamba katika Kikao kijacho cha Kamati ya Fedha na Utawala cha mwezi Novemba 2021 iwasilishwe taarifa ya hatua iliyofikiwa ya usajili wa shule ya Sekondari ya Itende na shule ya Sekondari ya Itagano.
3. Kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala kilijadili na kuazimia kwamba katika Kikao kijacho cha Kamati ya Fedha na Utawala cha mwezi Novemba 2021 ifanyike ziara ya kutembelea eneo linalotarajiwa kujengwa shule ya Sekondari Iyela.

**MCC/FU/04/2021/2022 (A) MAOMBI YA KUFANYA MABADILIKO YA VIFUNGU VYA FEDHA KIASI CHA TSH. 100,000,000/= KUTOKA MAPATO YA NDANI**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji ndugu Hajayand Adon aliwasilisha taarifa ya maombi ya kufanya mabadiliko ya vifungu vya fedha kiasi cha Tsh. 100,000,000/= kutoka Mapato

ya Ndani na kueleza kuwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya imepata udharula wa ukarabati wa miundombinu ya wafanyabiashara ndogondogo alimaarufu kama machinga katika maeneo mbalimbali na gharama ya ukarabati huo ni shilingi 100,000,000.00 kwa makadilio.

Mwisho aliomba Wajumbe wa Kikao cha Kamati ya Fedha na utawala kuidhinisha mabadiliko hayo ya vifungu ili kuwezesha shughuli ya ukarabati huu wa miundombinu kufanyika kwa wakati. Aidha alieleza kuwa fedha hizo zinatoka Idara ya Mipango, Takwimu na ufuatiliaji ambapo zilitengwa kwa ajili ya Ujenzi wa Hosteli eneo la Mzumbe.

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo, Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Utawala walipokea na kuridhia maombi ya kufanya mabadiliko ya vifungu vya fedha kiasi cha Tsh. 100, 000, 00.00 kutoka Mapato ya Ndani.

**MCC/FU/05/2021/2022 (B) UHAMISHO/KUONGEZA VIFUNGU KATIKA BAJETI ILI KUWEZA KUTUMIA FEDHA ZILIZOTOLEWA KWA AJILI YA KUTEKELEZA MRADI NA.5441- TANZANIA COVID – 19 SOCIAL ECONOMIC RECOVERY AND RESPONSE PLAN KUPITIA FEDHA ZA MKOPO NAFUU WA (IMF) INTERNATIONAL MONETARY FUND**

Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji ndugu Hajayand Adon aliwasilisha taarifa ya Uhamisho/kuongeza vifungu katika Bajeti ili kuweza kutumia fedha zilizotolewa kwa ajili ya kutekeleza Mradi Na.5441- "Tanzania Covid – 19 Social Economic Recovery and Response Plan" kupitia fedha za mkopo nafuu wa (IMF) "International Monetary Fund".

Alieleza kuwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya ilipokea barua yenye kumbukumbu namba Kumb. Na. CDC.66/109/03/35 ya tarehe 22/10/2021, yenye lengo la kufanya uhamisho wa nje ya Bajeti/ kuongeza vifungu kwa fedha zilizoletwa kiasi cha shilingi 1,840,000,000.00, kuomba kibali cha uhamisho wa fedha kutoka Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa na kuidhinisha uhamisho/kuongeza vifungu hivyo kupitia Kikao cha Kamati ya Fedha na Utawala.

Mwisho aliomba Wajumbe wa Kikao cha Kamati ya Fedha na utawala kuidhinisha uhamisho huo/ ongezeko hilo la vifungu vya kiasi cha Tsh.1,840,000,000.00 ili ziweze kutumika kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 92 vya madarasa katika shule 29 za Sekondari za Halmashauri ya Jiji. Aidha aliwasilisha orodha ya shule 29 za Sekondari zitakazokuwa na ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa kutumia fedha hizo.

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo, Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Utawala walipokea na kuridhia Uhamisho/Kuongeza vifungu katika Bajeti ili kuweza kutumia fedha zilizotolewa kwa ajili ya

kutekeleza Mradi Na.5441- Tanzania Covid – 19 Social Economic Recovery and Response Plan kupitia fedha za mkopo nafuu wa (IMF) International Monetary Fund.

**MCC/FU/6/2021/2022 KUFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili aweze kufunga Kikao.

Akifunga Kikao, Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe kwa kufanikisha kikao. Kikao kilifungwa saa 3:00 Asubuhi.

**Umethibitishwa**

| | |
|---|---|
| ................................ | ................................ |
| **Triphonia Kisiga** | **Mhe. Dormohamed I. Rahmat** |
| **Katibu** | **Mwenyekiti** |
| **Kamati ya Fedha na Utawala** | **Kamati ya Fedha na Utawala** |

**Tarehe.**15/11/2021